

HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA

MAFUNZO YA WAJUMBE WA KAMATI YA MAENDELEO YA KATA

(WDC) JUU YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA UFISADI,

YALIYOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI TAREHE

18/ 09/ 2017

WASHIRIKI WA WARSHA:

Washiriki waliokuwepo wameambatanishwa katika makundi kutoka katika taasisi zifuatazo

- | | |
|---|------|
| 1. Mkoani | (1) |
| 2. Mkuu wa Wilaya, Ngara | (2) |
| 3. Waheshimiwa Madiwani | (9) |
| 4. Wakuu wa idara | (14) |
| 5. Maafisa Utumishi | (5) |
| 6. Wawakilishi wa vyama vya Wafanyakazi | (2) |
| 7. Wawakilishi wa madhehebu | (2) |
| 8. Maafisa Tarafa | (2) |
| 9. Maafisa Watendaji wa Kata | (11) |
| 10. Maafisa Wtendaji wa Vijiji | (10) |
| 11. Klabu za kupambana na rushwa | (2) |
| 12. Ulinzi na Usalama | (4) |
| 13. Sekretarieti | (2) |

1. KUFUNGUA MAFUNZO

Afisa Utumishi wa Wilaya ya Ngara alisimamia zoezi la kutambulishana kwa washiriki, ambapo kila mmoja alijitambulisha kwa kutaja jina lake, kabla ya kumkaribisha Mkurugenzi Mtendaji wa Halmshauri. Mkurugenzi wa Wilaya alisisisitiza umuhimu wa washiriki kutumia nafasi hii,

kujielimisha kwa kushiriki kikamilifu kwa muda wote wa mafunzo, bila kutoka. Baada ya kusema hayo, Mkurugenzi wa Wilaya ya Ngasra alimkaribisha Mgeni rasmi, ambaye pia, ni Mkuu wa Wilaya ya Ngara. Hotuba ya ufunguzi kutoka kwa mgeni rasmi ilisheheni mambo ya msingi kama vile, washiriki kuzingatia na kuepuka chanzo cha kujihusishha na ufisadi ili kustawisha jamii, Mafunzo kujenga uwezo wa washiriki kuona namna ya kuzuia na kupambana na ufisadi kama ilivyoainishwa katika malengo ya Milenia, pamoja na kutafuta ya changamoto zinazokwamisha mapambano dhidi ya ufisadi.

2. UTANGULIZI

Muwezeshaji wa mafunzo haya alianza kwa kutoa ufanuzi kwamba, Mamalaka ya Serikali za Mitaa ilikuwepo kwa Mujibu wa sheria na japo, siyo Mamlaka zilizoko ndani ya Muungano.

3. MADA YA KWANZA: KUJUA MAJUKUMU YALIYOMO NDANI YA SHERIA YA MWAKA 1982 NA MABADILIKO YAKE YA MWAKA 2009

Mhadhiri kutoka chuo cha Serikali za mitaa alianza kwa kuwataka washiriki wote kutaja matarajio yao kama washiriki wa Semina. Matarajio mbalimbali yaliorodheshwa na washiriki kama ifuatavyo: kupata namna bora ya kudhibiti ufisadi, kuelewa athari za ufisadi, kuongeza uelewa juu ya sheria husika kudhibiti ufisadi na kuandaliwa kuwa muadilifu na kuelewa kiwango na hali halisi ya ufisadi

Vilevile mwezeshaji aliweza kutoa wasaa wa kila mshiriki kutaja kuonesha namna alivyokuwa amelielewa na kulichukulia zoezi la kutaja matarajio ya washiriki kwa ujumla. Miongoni mwa wajumbe walionesha uelewa wao kuwa ni pamoja na; kila mmoja alikuwa na jinsi alivyofahamu maana ya ufisadi, kila mmoja alionesha nia ya kupata mafunzo haya, wahiriki walikuwa tayari kupokea wajumbe na kuwa, washiriki wote nwalikuwa wanakubaliana kwamba ufisadi siyo lazima kiwe ni kitu kikubwa bali vitu vidogo vidogo ambavyo viko katika maisha yetu ya kila siku.

Hata hivyo, mwezeshaji aliweza kutoa ufanuzi na kusisitiza kuwa, washiriki wote, bila kujali cheo, umri, kabilia, idara, dini au rangi alikuwa na jukumu la kushiriki kikamilifu kwani

walikuwa wanajenga nyumba moja. Alimalizia kwa kusisisitiza kuwa, kila mmoja alikuwa na mchango unaothaminiwa katika mafunzo hayo. Hivyo, asisite kutoa mawazo yake kwa wengine.

4. MUUNDO WA MAMLKA ZA SERIKALI ZA MITAA

Mada hii ilianza kwa maelezo kwamba, mfumo wa Serikali za Mitaa ulikuwa ni wa kikatiba, ambapo majukumu yake yalikuwa yametajwa na kuelezwa katika Mamlaka zote za Serikali. Mamlaka ya Serikali za Mitaa siyo suala la Muungano! Taarifa ya Mwezeshaji ilimalizia kwamba, ndio maana hutumia miongozo na sheria mbalimbali.

Aidha Ilisisitizwa kuwa, madhumuni ya jumla ya kuanzisaha serikali za mitaa yalikuwa na mizizi yake katika kupeleka huduma bora kwa wananchi kwa kuzingatia; Madaraka kwa wananchi, kutoa haki na mamlaka ya kuwashirikisha wananchi katika mipango, kutekeleza na kusimamia kazi za Serikali za mitaa katika eneo husika, kuimarisha sheria na ulinzi wa wanancni, pamoja na kuimarisha demokrasia.

Vilvile, ilielezwa kwamba, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimegawanyika katika makundi makuu mawili, kimsingi, ambayo yalitajwa kuwa ni; Mamlaka za Miji na Majiji zenyenye Kata hadi Mtaa na Mamlaka za Wilaya zenyenye Kata, Kijiji na Kitongoji.

5. KAMATI ZA MAENDELEO YA KATA

\Ilielezwa kwamba kamati hizo zilikuwa zimeanzishwa chini ya sheria namba 7 na 8 ya mwaka 1982 ambapo Wajumbe walikuwa wameainishwa katika kifungu namba 32. Kamati hizi zilitajwa kuwa ni kamati za uratibu za misingi (kiungo) na hujadili masuala yote ya maendeleo katika vijiji vya maeneo ya kata husika. Wajumbe hawawaliainishwa kama ifuatavyo:

- Mbunge au wabunge wa kuchaguliwa na wakazi wa kawaida ndani ya kata
- Diwani (Mwenyekiti)
- Afisa Mtendaji wa Kata (Katibu)
- Wenyeviti wa Vijiji katika husika

Aidha, Mwezeshaji alisisitiza kwamba vikao vya Kamati ya maendeleo ya Kata hutakiwa kukutana mara nne kwa mwaka japo vikao vya dharula vimeruhusiwa.

Katibu wa kikao hutakiwa kuandika taarifa na kuhakikisha utekelezaji wa maamuzi na sera za Halmashauri husika pamoja na majukumu yafuatayo

- ✓ Kuwezesha uanzishwaji wa taasisi na shuguli za ushirika ndani ya kata
- ✓ Kupanga na kuratibu shughuli mbalimbali
- ✓ Kusimamia pesa zote
- ✓ Uanzishwaji wa Serikali za vijiji
- ✓ Kupambana na majanga na shughuli za mazingira
- ✓ Kusimamia ukusanyaji wa mapato ili kuimarisha miundo mbinu kulingana na mahitaji ya kila mkazi
- ✓ Kuwashirikisha kikamilifu watendaji wa idara zote kuleta maendeleo ya wananchi

Katika kuhitimisha mada hii, msisitizo ulitiliwa kwenye maana ya Maendeleo ni ubora wa mifugo, barabara na barabara kuu, majengo ya ustawi wa jamiii na ujenzi wowote na miradi amabayo hutakiwa kuthibitishwa na mkurugenzi wa Halmashauri husika, kwa kufuata utaratibu wowote kupitia vikao na mikutano ya hadhara.

Kwa ujumla, washiriki walivutiwa na kufurahishwa na jinsi muwasilishaji alivyowashughulisha katika mada kwa kutumia vitendo mbalimbali, hususani wimbo wa “Tanzania Tanzania”.

6. MADA YA PILI: MADHARA YA KUJIHUSISHAS NA UFISADI

Mambo ya msingi yaliyosisitizwa wakati wa uwasilishwaji wa mada hii ni kama ifuatavyo:

- Kriminolojia- kufanya utafiti wa kwanini watu hukosa uadilifu, hali ambayo inatawaliwa na maswali mengi ya kwanini, ubayana wa uhalifu na kwa kuwa kuna imani kwa binadamu siyo wasafi kwa asili yao
- Maana ya ufisadi ilitolewa kulingana na vikundi mbalimbali kama vilivyoundwa katika ukumbi. Majibu yaliyoletwa kulingana na makundi mawili, ambapo majina yaliweza kutengwa kulinga na majina mazuri na majina mabaya kama kielelezo cha tabia za mafisadi.

Washiriki katika makundi hayo waliweza kubainisha kuwa kwa upande mmoja majina mazuri ni Ng'ombe ambaye ana faida nyingi kwa binadamu kama vile kutoa nyama, maziwa, na ngozi amba hudhihirisha viongozi wanaofanya kazi sana, Kondoo ambaye ni mpole kwa ujumla lakini mwenye kasi kubwa katika kumkwepa adau, Mbuzi mwenye kuhitaji umakini, Bata ambaye hutembea mbele wakati vifaranga vyake viko nyuma na hivyo nirahisi vifaranga kuibwa bila habari, na hatimaye paka.

Kwa upande wa Majina mazuri yaliyotajwa ni pamoja na Ngedere aliyetajwa kuwa mharibifu wa kila aina ya zao, chui kama na samba ambao ni wanyama wanaotajwa kuwa wakali kiasi cha kutoaminiwa na kila mmoja, kunguru ambaye ni mnyama mdokoz tu, Mwewe ambaye sifa yake ni kufacha wanawe na kwenda kuhujumu vifaranga wa kuku na fisi ambaye alitajwa kuwa ni mzembe asiyeweza kuhangaika kujitafutia kwa kujitegemea.

Majadiliano kwa ujumla yalisitsitiza kwamba kila jambo huweza kuwa na faida na hasara, Hivyo, kiutendaji ni vema kuangalia pande zote na mkutadha husika kwa namna ya kupambana na ufisadi: kutoa huduma, kubainisha nani ni fisadi, Viashiria vya ufisadi,

Aidha maana za rushwa zilionekana kuwa katika kutoa na kupokea hongo ili mhusika apate upendeleo japokuwa bila sifa na kufanya mambo kinyume cha utaratibu katika mazingira maalum

Kwahiyo, washiriki wote wametakiwa kupambana na hali hiyo kwa nguvu zote za pamoja,

Ufisadi kwa upande mwingine ultafutiwa m'aana yake na maana zifuatazo zilibainishwa na washiriki katika mafunzo haya: Matumizi mabaya ya rasilimali kama vile, mdaraka, muda, mali na kujilimbikizia maali, na ama fedha. Matendo yanayoweza kusababisha mambo Fulani yasiweze kutekelezwa, kupunguza malengo yaliyokusudiwa wakati gharama zikibaki kuwa za juu, utamaduni wa mtu mmojammoja.

Vile, idra zinazoongoza kwa vitendo na viashiria vya ufisadi ni pamoja n Elimu, Mahakama, TAKUKURU, Polisi na magereza, Mabaraza ya kata na Ardhi, Afya

Sababu zinazosababisha mianya ya ufisadi zilitajwa kuwa ni pamoja na nammna motisha zinavyotolewa: Fursa zinavyotolewa kulingana na msukumu ulivyotolewa na namna ya uhalarishaji wa watu katika nafasi zao.

Kwa hiyo, hayo yote yakiondolewa kwa pamoja bila kuacha hata moja, ufisadi utapungua kama siyo kuisha kabisa.

Baada ya majadiliano hayo kukamilika, majadiliano ya awamu ya pili yalianza baada ya kuundwa kwa vikundi vitatu ili kila kikundi kijadili mojawapo kati ya namna motisha zinavyotolewa, Fursa zinavyotolewa na namna ya uhalarishaji.

7. CHAKULA CHA MCHANA

Washiriki wote walipata chakula kuanzia saa 8.30 mchana hadi 9.20 za mchana.

8. MAJADILIANO YA AWMU YA PILI: MIHIMILI YA UFISADI

Baada ya chakula cha mchana kila kikundi kilifanya majadiliano, kisha kufanya uwasilishaji ambao ulifanyika kama ifuatavyo;

Fursa/ Mianya

Mhimili huu ulijadiliwa na kundi la kwanza na kuibuka na mawazo kama;

Kundi la kwanza liwasilisha kuwa mianya iliyopo ni pamoja matumizi ya madaraka, raslimali zisizokidhi haja, usimamizi hafifu, udhaifu wa sheria, uelewa mdogo juu ya haki stahiki kwa raia na majanga au maafa.

Washiriki kwa pamoja walipokea mawzo ya wanakikundi hicho na kuyapitisha kwa kukubaliana kuwa ni kweli yako katika jamii yetu. Kwa hiyo, ni vema viongozi wakawa makini katika namna ya kumiliki madaraka yao katika kulinda raslimali za jamii. Aidha, sheria zinatakiwa zibadilishwe mara kwa mara. Huku wakuu wa taasisi wakitakiwa kuhakikisha wana jamii wana uelewa wa juu wa sheria.

Msukumo (Pressure):

Mhimili huu, ulijadiliwa na kuwasilishwa na kundi la pili amvpo, washiriki walisisisitiza kwamba misukumo inayopelekea kuwepo kwa ufisadi ni pamoja na; tama, maisha yasiyolingana na kipato, ushwishi wa makundi, tabia na hulka binafsi za baadhi ya watu na mazingira ya upatikanaji au uhitajiwa huduma.

Mambo mengine yanayosukuma mtu kujihusisha na ufisadi yalitajwa kuwa pamoja na haki, matatizo ya kukidhi mahitaji ya familia, uhitaji wa kuendana na wakati, uelewa mdogo wa kisheria, uoga wa kisheria na kipato kisichowenza kukidhi mahitaji.

Washiriki walipokea mawazo ya kikundi na kufanya marekebisho kuwa matatizo ya kifamilia ni mengi, hivyo kila mmoja ajaribu kuyaainisha vivilivo, Vilevile, ilielezwa kwamba, utamaduni nao umechangia kwa wengi kujiingiza katika shughuli za ufisadi, kama ilivyo asili ya baadhi ya watu katika jamii.

Washiriki baada ya uwasilishaji huo walikubaliana na hoja kwamba Elimu pekee itatumia kuwabdalisha watu wenye elementi za ufisadi..

Uhalalishaji

Mhimili huu ulijadiliwa na kuwasilishwa na washiriki katika kundi la tatu kwa kusema kwamba, mambo yanayopelekea uhalarishaji wa matendo ya ufisadi ni pamoja na, tamaa ya kuishi zaidi ya kipato chake, tabia/ mazoea, kukosa uadilifu na uaminifu, mfumo mbovu wa uendeshaji kwa kutumia sheria zisizokuwa na meno, ukiuwaji wa sheria, kanuni na taratibu na hali ngumu ya maisha.

Baada ya washiriki kupokea mawazo ya kikundi, washiriki wengine, waliongeza kwamba katika kupambana na ufisadi haipaswi watu kuaminiana kwa namna yoyote.

Baada ya uwasilishaji huo, ilisisitizwa kuwa ni vizuri kuielewa kwa kina mihimili hiyo ili kupambana na ufisadi katika jammii zetu na Tanzania kwa ujumla.

SHERIA YA PCA, PENAL CODE, PCCA, CODE OF ETHICS AND CONDUCT FOR PUBLIC SERVICE, PUBLIC LEADERSHIP, PUBLIC SERVICE ACT, AND PUBLIC PROCUREMENT ACT.

Washiriki waliwekwa katika makundi ili kujadili sheria hizo. Wakiwasilisha matokeo ya mjadala huo, mawazo yao yaliwasilishwa kwa kwa kuonyesha faida mna mapungufu kama ifuatavyo:

Kundi la kwanza;(Madiwani na Madiwani)

Kundi la Pili (Waalimu na wanafunzi)

Kundi la tatu; (Madhehebu

Kundi la nne (Vyombo vyat ulinzi na usalama)

Kundi tano (Wakuu wa idara)

Baada ya washiriki kupangwa katika makundi hayo, wajumbe wlikubaliana na hojaya kuanza na mada hii siku ya kesho yake ya tarehe 19/09/2017.

Baada ya makubaliano hayo ilitangazwa mafunzo ya kesho yake yangeanza kunako saa 2.00 za asubuhi